TANGAZO LA SERIKALI Na. 222 la Tarehe 29/2/2024

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 153)*

SHERIA NDOGO ZA VIBALI VYA UJENZI ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA ZA MWAKA 2024

Jina

**1**. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za Vibali vya Ujenzi za Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga za Mwaka 2024.

Matumizi

**2**. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika maeneo yote yaliyopo katika mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga na hazitahusisha Ujenzi wa Majengo ya Serikali au Mashirika ya Umma.

Tafsiri

**3**. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Ada" maana yake ni kiwango cha fedha kinakachotozwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni afisa wa Halmashauri aliyeidhinishwa na Mkurugenzi kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga;

"jengo la makazi" maana yake ni jengo kwa madhumuni ya shughuli na huduma zisizo za"jengo la biashara" maana yake ni jengo kwa madhumuni ya biashara na shughuli zote zinazoambatana na biashara; kibiashara;

"Kibali" maana yake ni ruhusa au ridhaa ya maandishi kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga; na

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga ikijumuisha afisa yoyote wa Halmashauri anayekaimu wadhifa wa Mkurugenzi.

Masharti ya ujenzi

**4**.-(1) Ni marufuku Mtu kuanza ujenzi au shughuli zozote zinazoambatana na ujenzi ndani ya mamlaka ya Halmashauri bila kupata kibali halali cha ujenzi husika kutoka Halmashauri na Maombi ya kibali cha Ujenzi ni kama yalivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

(2) Kibali cha ujenzi kitatolewa kwa kuzingatia ramani ya jengo husika kama itakavyowasilishwa katika Halmashauri na mhusika wa ujenzi.

(3) Kibali cha ujenzi hakitatolewa kwa Mwombaji wa kibali mpaka atakapokuwa amelipa ada kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

Uwezo wa kuingia

**5**. Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hizi, Afisa Mwidhinishwa atakuwa na mamlaka ya kuingia katika kiwanja chochote ambacho ujenzi unafanyika kwa nia ya kujiridhisha kama ujenzi huo umepata kibali kutoka Halmashauri.

Faini na adhabu

**6**.-(1) Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kumtoza faini mtu ambaye atabainika kukiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi.

(2) Mtu atakayebainika kuanza au kuendeleza ujenzi bila ya kibali cha ujenzi kutoka Halmashauri, atawajibika kubomoa ujenzi huo kwa gharama zake mwenyewe.

(3) Bila ya kuathiri aya ndogo 1 na 2 ya aya hii, mtu atakayekiuka au kuvunja masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozisi shilingi Milioni Moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne, au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Wajibu wa Halmashauri

**7**. Halmashauri itakuwa na wajibu wa kulipa fidia kwa hasara yoyote itakayosababishwa na Afisa Mwidhiniwa au Afisa yoyote wa Halmashauri kutokana

na uzembe au kwa makusudi wakati wa utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

Kufifilisha Kosa

**8**. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Tatu.

JEDWALI LA KWANZA

(*Limetengenezwa chini ya aya ya 4(3)*)

ADA YA UJENZI

| Namba | Aina ya Jengo | Ada ya Ukaguzi | Ada ya Kibali |
|---|---|---|---|
| 1 | Ghorofa 1 | 50,000 | 100,000 |
| 2. | Ghorofa 2 na kuendelea | 50,000 | 150,000 |
| 3 | | | |
| 4 | Ghala au Bohari | 50,000 | 100,000 |
| 5 | Kituo cha Mafuta | 50,000 | 200,000 |
| 6 | Nyumba za Makazi | 20,000 | 30,000 |
| 7 | Nyumba za Makazi na Biashara | 30,000 | 50,000 |
| 8 | Uzio wa Sengenge | 10,000 | 25,000 |
| 9 | Uzio wa Ukuta | 20,000 | 40,000 |
| 10 | Minara ya Mawasiliano | 200,000 | 300,000 |
| 11 | Marekebisho ya Jengo | 10,000 | 30,000 |
| 12 | Majengo ya Shule au Taasisi Binafsi | 50,000 | 200,000 |
| 13 | Majengo mengine ambayo hayakutajwa hapo juu<br>i)Jengo dogo<br>ii) Jengo Kubwa | <br>20,000<br>100,000 | <br>30,000<br>200,000 |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(1))*

SEHEMU YA KWANZA

FOMU YA MAOMBI YA KIBALI CHA UJENZI

TAARIFA FUPI YA MWOMBAJI

Jina la Mwombaji ………………………………………………….

Anuani ……………, …………………

Namba ya Simu …………………………..

Barua pepe ……………………………………………

AINA YA JENGO LINALOTARAJIWA KUJENGWA

Jengo linalojengwa (Ghorofa/Kawaida/Uzio/Ukuta/Marekebisho (taja)………...............................

Kama Ghorofa (taja ngapi) ……………….

Ramani ipo (ndiyo/hapana) ……………... (ni muhimu iwepo na iambatanishwe na fomu ya maombi)

Saini ya mwombaji ………………………………………..

Jina la mwombaji …………………………………………….

Angalizo-Gharama za maombi ya Kibali cha Ujenzi hazitarejeshwa hata kama mwombaji atakuwa amekosa kuidhinishiwa maombi yake.

MAHALI ANAPOTAKA KUJENGA MWOMBAJI (ajaze afisa wa serikali)

Mtaa/kijiji ……………………………..
Kata ………………………………..
Namba ya simu ya Afisa Mtendaji Mtaa/Kijiji/Kata …………………………
Eneo limepimwa/halijapimwa …………………………….

Mhuri na Saini………………………………………………………
Jina la Afisa Mtendaji …………………………………………………

*Tangazo la Serikali Na.222 (Linaendelea.)*

SEHEMU YA PILI
FOMU YA MAONI YA KIBALI CHA UJENZI

Maombi ya Ndugu ……………………………………………………
Fomu Na. ………………..
Maoni ya Kitaalamu
Mkaguzi wa Majengo, (toa maoni ya kitaalamu apewe/asipewe. Na kama asipewe kwa nini) ……………………………………………………………………
Jina ……………………………….Saini……………Tarehe …/…/20…
Afisa Ardhi, (toa maoni ya kitaalamu apewe/asipewe. Na kama asipewe kwa nini) …………………………………………………………………………
Jina ……………………………Saini……… Tarehe …../…../20..…..
Mpima Wilaya, (toa maoni ya kitaalamu apewe/asipewe. Na kama asipewe kwa nini) …………………………………………………………………………
Jina ……………………………Saini……………Tarehe …../..…/20..…
Afisa Mipango Miji, (toa maoni ya kitaalamu apewe/asipewe. Na kama asipewe kwa nini) …………………………………………………………………………
Jina …………………………Saini……………Tarehe …../..…/20..…
Afisa afya, (toa maoni ya kitaalamu apewe/asipewe. Na kama asipewe kwa nini) …………………………………………………………………………
Jina …………………………Saini……………Tarehe …../..…/20..…

Maoni yamepokelewa kwa Mhandisi leo Tarehe …/…/20..…

Jina …………………………………………..Sahihi……………………

Kibali ……….

S/N MDC …………/20…..

SEHEMU YA TATU

KIBALI CHA UJENZI

Kibali kinatolewa kwa Ndugu. …………………………………..........
Kibali Na. ……………kimeidhinishwa na Kamati ya Mipango miji na Mazingira katika kikao cha Tarehe ……../………/20……
Kujenga Nyumba ya kawaida/Uzio/Kufanya marebisho/Nyumba ya Ghorofa……………… (taja idadi na aina ya matumizi) ………………
Katika kiwanja Na……….. Kitalu…………kilichopo.……………………

Kulingana na Ramani zilizoambatanishwa pamoja na masharti yote yaliyoambatana na Kanuni ya Ujenzi
Unatakiwa Upande Miti isiyopungua mitano ya matunda au kivuli katika kiwanja chako katika Harakati za kuboresha Mazingira. Pia utafuata Sheria zote ikiwa ni pamoja na kukaguliwa na Mhandisi wa Ujenzi wa Wilaya kwa hatua zote za Ujenzi.

Kibali hiki kitadumu kwa muda Miaka mitatu ya Ujenzi, na ndani ya Miezi sita unatakiwa uwe umeanza kuendeleza/kujenga kuanzia Tarehe ya kibali kilipotolewa. Vinginevyo kibali hiki kitakuwa BATILI
Kibali kimetolewa leo Tarehe …………/…………/20………….

Saini ………………………………….

MKURUGENZI MTENDAJI
HALAMASHAURI WILAYA YA MWANGA

Nakala;
Afisa Mtendaji Kata
………………………..

JEDWALI LA TATU

(*Limetengenezwa chini ya aya ya 8*)

FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ……………………………………………………… nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya …………………………………………. ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga, kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……. Mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya Sheria Ndogo ya Vibali vya Ujenzi ya Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga ya Mwaka, 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga, niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini badala ya kushtakiwa Mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe…………. ya Mwezi…………..… Mwaka …………….
Jina……………………………….. Saini………………………
MBELE YANGU:
Jina: …………………………………..……………
Saini ……………………….………………………
Wadhifa: ………………………………………………
Tarehe …………………………………………………

Lakiri ya Halmashauri ya Manispaa ya Mwanga imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio la mkutano wa Baraza la Halmashauri ya ya Wilaya ulioitishwa na kufanyika tarehe 1/3/2023, mbele ya:-

MWAJUMA A. NASOMBE,
*Mkurugenzi mtendaji,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Mwanga*

MHE. DR.SALEHE R. MKWIZU,
Mwenyekiti,
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Mwanga*

L.S

NAKUBALI,

Dodoma,
30 Januari, 2024.

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi OR-Tamisemi*